



## TAARIFA KWA UMMA

### KUSUDIO LA KUCHUKUA HATUA DHIDI YA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI YANAYOJIENDESHA KINYUME CHA SHERIA

Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali anakusudia kuyachukulia hatua Mashirika yanayoendesha shughuli zao kinyume cha Sheria ya NGOs Na. 24 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebisha mwaka 2005. Mashirika hayo ni yale ambayo hayajawasilisha taarifa za mwaka kwa kipindi cha miaka miwili pasipo kutoa sababu za msingi, kulipa ada ya mwaka au kuendesha shughuli za NGOs bila kusajiliwa chini ya Sheria ya NGOs.

Kwa taarifa hii, Mashirika husika yanatakiwa yawe yamerekebisha dosari tajwa ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Baada ya kipindi hicho, Msajili wa NGOs atayafutia usajili Mashirika ambayo yatakuwa hayajawasilisha taarifa na kuyachukulia hatua stahiki Mashirika yanayoendesha shughuli za NGOs bila ya usajili chini ya Sheria husika.

Malipo yote ya ada yafanyike kupitia **Benki ya NMB, NGO Account Na. 20110014074** na stakabadhi halali ya malipo itumwe kwa Msajili wa NGOs.

Imetolewa na,

M.S. Katemba

**MSAJILI WA NGOs**

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

06 Januari, 2016